**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**

**22 Oktoba, 2025**

# TANGAZO KWA UMMA KUHUSU UPIMAJI WA KITAIFA DARASA LA NNE 2025

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha inawatangazia umma kuwa upimaji wa kitaifa wa darasa la nne utafanyika Tarehe 22 Oktoba, 2025 na Tarehe 23 Oktoba, 2025 ambapo Wilaya ya Siha ina jumla ya shule za msingi 59 za serikali na 14 za binafsi.

Kwa mwaka 2025, Jumla ya Watahiniwa 3176 wamesajiliwa kufanya upimaji huo kwa Wilaya nzima ambapo kati ya hao wavulana ni 1535 na wasichana ni 1641.

Mtihani huo unafanyika kwa mfumo wa Kiswahili na mfumo wa Kiingereza ambapo watahiniwa wa mfumo wa Kiswahili watakua 2722 kati ya hao wavulana ni 1303 na wasichana ni 1419.

Watahiniwa wa mfumo wa Kiingereza watakuwa 454 ambapo wavulana ni 232 na wasichana ni 222.

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji inatoa rai kwa wazazi na walezi kuwapa ushirikiano watahiniwa hawa ili waweze kushiriki vema kufanya upimaji wao.

**Imetolewa na;**

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini,**

**Halmashauri ya Wilaya ya Siha**

**Oktoba 22, 2025**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, 5 BR Sanya Juu - Elerai, S.L.P. 129, 25482 Siha - Kilimanjaro
Simu: 0272-970677 Nukushi: 027-2970678
Baruapepe:ded@sihadc.go.tz  Tovuti:www.sihadc.go.tz